JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI SOVI,
S.L.P 849,
NJOMBE.

KUMB. NA. SVSS/JINS/3/15
……..
…….
…….
Ndugu,

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umecahaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Sovi. Nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari katika shule hii. Hii ni bahati ya pekee uliyoipata katika wachache, wewe ukiwa mmojawapo. Ni matumaini yangu kuwa utaikubali na kuitumia nafasi hii vizuri kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za shule.

1. **MAZINGIRA YA SHULE.**

Shule ya sekondari Sovi ipo katika kata ya Mtwango ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Vijijini. Shule hii ni ya mchanganyiko yaani wavulana na wasichana.

2. **TAREHE YA KUWASILI SHULENI.**

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**. Fika katika ofisi ya Mkuu wa shule ukiongozana na mzazi/mlezi wako ili uweze kupokelewa na kusajiliwa rasmi.

3. VIFAA VYA MASOMO.

a) Mkebe wa Hisabati (Mathematical Set) - 1
b) Daftari kubwa zenye ganda gumu (Counter books) Quire Two - 12
c) Kalamu za wino (pen) - 5
d) Kalamu za risasi (pensel) - 2 pamoja na viambata vyake yaani kichongeo na kifutio.
e) Rula
f) Mfuko au begi la shule kwaajili ya kutunzia vifaa vya shule.
g) Dictionary (Kamusi ya Kiingereza – Kiingereza)
NB. Vifaa vingine utaendelea kuagizwa kadiri utakavyoendelea na masomo.

4. MAHITAJI MENGINE

4.1 SARE ZA SHULE

i. WAVULANA

- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
- Suruali mbili za rangi ya **Damu ya mzee** na **Nyeusi**; ambapo damu ya mzee itavaliwa siku ya Jumatatu na Jumanne na nyeusi itavaliwa siku ya Jumatano na Alhamisi; na siku ya Ijumaa atavaa truck suit na T-shirt.
- Aina ya vitambaa vya suruali hizo ni **ISTIMU** na siyo vinginevyo. Suruali hizo ziwe na **TURN UP** yaani upindo wa chini ya suruali na usiopungua inchi 18.
- Sweta mbili za rangi ya kijani jeshi
- Viatu vyeusi vya ngozi, vyenye kamba na visigino vifupi.
- Mkanda wa ngozi mweusi wenye upana usiozidi inchi 2
- Soksi za rangi nyeusi jozi mbili.
- Truck suit nyeusi (1) itakayovaliwa siku ya Ijumaa (siku ya michezo)
- T- shirt ya rangi ya bluu iliyokolea aina ya **Babalance**

ii. WASICHANA.

- ✓ Shati mbili nyeupe za miko mifupi.
- ✓ Suruali mbili za rangi ya Damu ya mzee na Nyeusi; ambapo damu ya mzee itavaliwa siku ya Jumatatu na Jumanne na nyeusi itavaliwa siku ya Jumatano na Alhamisi; na siku ya Ijumaa atavaa truck suit na T- shirt.
- ✓ Aina ya vitambaa vya suruali hizo ni ISTIMU na siyo vinginevyo. Suruali hizo ziwe na **TURN UP** yaani upindo wa chini ya suruali na usiopungua inchi 18
- ✓ Magauni mawili ya rangi zinazo fanana na suruali (damu ya mzee na nyeusi) na kitambaa kiwe ni aina ya **ISTIMU**. Aidha tumeambatanisha na mchoro unaoonesha namna ya kushona magauni hayo pamoja na sheria na kanuni za shule.
- ✓ Sweta mbili za rangi ya kijani jeshi
- ✓ Viatu vya ngozi vyeusi, vyenye kamba na visigino vifupi.
- ✓ Soksi za rangi nyeupe jozi mbili.
- ✓ Truck suit nyekundu (1) itakayovaliwa siku ya Ijumaa (siku ya michezo)
- ✓ T- shirt ya rangi ya bluu iliyokolea aina ya **Babalance**

Pamoja na fomu hii tumeambatanisha vijipande vya vitambaa kwaajili ya suruali/sketi na sweta

NB: *MWANAFUNZI ANAPOKUJA KURIPOTI AWE AMEVAA TRUCK SUIT, NA SARE ZINGINE ZIBEBWE KWA AJILI YA UKAGUZI.*

5. UJAZAJI WA FOMU NA NAKALA MUHIMU ZA KUWASILISHA SHULENI.

Kabla ya kuripoti shuleni hakikisha umejaza fomu zilizo ambatanishwa na maelekezo haya ambazo ni:-

a. Fomu ya kukubali kuendelea na masomo ya sekondari (Mkataba)
b. Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi.
c. Fomu ya vipimo vya kiafya (Medical Examination)
d. Pamoja na fomu hizo ni muhimu kuwasilisha nakala za Bima ya afya na cheti cha kuzaliwa au barua ya uthibitisho kutoka kwa ofisi ya kijiji unachoishi (kwa asiye na cheti cha kuzaliwa)

KARIBU SANA.
ELIMU KWA MAENDELEO.

Wako
BARTHOLOMEW J. MHEMA

MKUU WA SHULE

SARE YA SAUTI YA SEKONDARI

YA WASICHANA



JAMUHUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI SOVI
SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mwanafunzi yeyote anatakiwa kufuata sheria za shule kama ifuatavyo

a. Kuhudhuria masomo kila siku. Kama kuna tatizo la ugonjwa, kufiwa n.k lazima mwanafunzi aombewe ruhusa na mzazi/mlezi.
b. Kuwasalimia na kupokea mizigo watu wote waliomzidi umri.
c. Kusalimia mwalimu aingiapo darasani na wakati wa kujibu maswali.
d. Kufika shuleni kabla ya saa 1:00 asubuhi na kufanya usafi katika eneo alilopangiwa.
e. Kukubali adhabu zinazotolewa na walimu shuleni au viranja. Kukiwa na swali liulizwe baada ya kutekeleza adhabu.
f. Kuvaa nguo ndefu na za heshima yaani zisizobana au kuangaza wakati wote uwapo shuleni au nyumbani.
g. Kuheshimu bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa na wimbo wa shule.
h. Kutunza mazingira ya shule.
i. Kutopiga kelele darasani.

NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI.

i. Kutumia lugha chafu, matusi au lugha ya kashfa.
ii. Kutembelea nyumba za kulala wageni (Guest house),vilabu vya pombe,nyumba za walimu na vibanda vya kamali.
iii. Kufuga nywele ndefu, ndevu, kucha, kuvaa mikufu,heleni,bangili,kupaka wanja, piko kutumia marashi.
iv. Kumiliki simu au laini ya simu,kamera au redio wakati wote awapo shuleni.
v. Kujihusisha na mapenzi kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au mtu yeyote asiye mwanafunzi.
vi. Kuondoka shuleni kabla ya muda wa masomo kumalizika yaani kabla ya saa 9:30 jioni.
vii. Kuvaa kofia maeneo ya shule.
viii. Kunyoa nywele zote na kuacha kipara au kunyoa kwa namna inayoashiria uhuni.

MAKOSA YATAKAYOMFUKUZA MWANAFUNZI MARA MOJA NI PAMOJA NA:-

1. Wizi.
2. Uasherati,ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya pombe,uvutaji wa bangi, matumizi ya madawa ya kulevya au kubeli.
4. Kucheza kamali.
5. Kutenda makosa ya jinai .
6. Kupiga au kupigana pamoja na kuchochea ugomvi.
7. Kuoa au kuolewa
8. Kupata mimba au kusababisha mimba .
9. Kutoa au kusaidia kutoa mimba.
10. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa
11. Kuwagomea walimu, wafanyakazi wa shule ,viongozi wa serikali au kufanya kitendo chochote cha kuanzisha,kushiriki au kuchochea mgomo.
12. Kusababisha uvunjifu wa amani shuleni.

THE PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

SOVI SECONDARY SCHOOL

P.O BOX 849

NJOMBE.

REF. NO. SVSS/1/INS/01/15

THE MEDICAL OFFICER,

……

……

……

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please kindly examine (Name)

……..

To determine his/ her physical and mental fitness for pursuing secondary studies.

BARTHOLOMEW J. MHEMA

HEADMASTER

1. Eye sight ……..
2. Hearing ……...
3. Speech …….
4. Limbs ……
5. Leprosy ……
6. Epilepsy …….
7. Cardiac diseases……
8. Rheumatism ……..
9. Venereal diseases ……..
10. Pregnancy (for girls)……
11. Any serious diseases……..

General comments……

……

Signature …… Date …….

Stamp ……

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kimili la mwanafunzi ……
2. Tarehe ya kuzaliwa ……
3. Mahali alipozaliwa: Kijiji/ Mtaa ……..

   Kata …….. Wilaya……
4. Dini …… Dhehebu ……..
5. Jina la baba…….

   Baba ni mzima? (Ndiyo / Hapana)

   Kazi yake ……
6. Jina la mama……

   Mama ni mzima? (Ndiyo / Hapana)

   Kazi yake……

   Namba ya simu ya mzazi mmojawapo ……

IWAPO HANA WAZAZI

7. Jina la mlezi……. (Mme/ Mke)
8. Kazi yake ……..
9. Uhusiano wake na mlezi…….
10. Taja ndugu wawili wa karibu nawe kimalezi

    …… Namba ya simu……..

    …….. Namba ya simu……..

FOMU YA KUKUBALI KUENDELEA NA MASOMO (MKATABA)

(Ijazwe na mwanafunzi pamoja na mzazi/mlezi)

A. MWANAFUNZI

Mimi ……..

Naahidi kwamba niko tayari kusoma kwa bidii na nitatii sheria zote za shule kwa hiari yangu mwenyewe.

Saini …… Tarehe…….

B. MZAZI/MLEZI

Mimi ……..

Ambaye ni mzazi/ mlezi wa …… naahidi kwamba niko tayari kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma na kitabia pamoja na kumpa mahitaji yake yote muhimu ya shule (sare za shule, chakula, vifaa vya shule n.k)

Saini …… Tarehe…….

C. UTHIBITISHO WA OFISI YA KIJIJI ATOKAKO MWANAFUNZI

Nathibitisha kuwa mwanafunzi(andika jina)……

Anatoka katika kijiji cha…… (andika jina la kijiji). Hivyo naomba apokelewe.

Jina …….. Saini …….... Tarehe……..

Cheo ……

Muhuri